

# Nishani ya patakatifu (Sanctuary)

Nishani hii ipo katika kundi la spiritual growth, outreach & heritage (makuzi ya kiroho kuwafikia wengine na urithi wa kanisa), huwakilishwa kwa rangi ya bluu




By: Yusuph Mwasiposya

---

Sanctuary → Patakatifu.

Patakatifu:

*mahali, au kitu kilichotengwa kwa matumizi maalum.*

## Vifuniko vya hekalu:

- **Mapazia ya kitani safi.**

**Kisha fanya hiyo maskani iwe na mapazia kumi; ifanye ya nguo ya kitani nzuri ya kusokota, pamoja na nyuzi za rangi ya samawi, na ya zambarau, na *nyekundu*, pamoja na makerubi; kazi ya fundi stadi.**

**Kutoka 26:1**

---

## Vifuniko vya hekalu:

**Nyekundu huwakilisha Damu ya Yesu msalabani**

**wala si kwa damu ya mbuzi na ndama, bali kwa damu yake mwenyewe aliingia mara moja tu katika Patakatifu, akiisha kupata ukombozi wa milele.**

1 Petro 1:18:19

**Nanyi mfahamu kwamba mlikombolewa si kwa vitu viharibikavyo, kwa fedha au dhahabu; mpate kutoka katika mwenendo wenu usiofaa mlioupokea kwa baba zenu; bali kwa damu ya thamani, kama ya mwana-kondoo asiye na ila, asiye na waa, yaani, ya Kristo.**

Ebrania 9:12

---

## Vifuniko vya hekalu:

**Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.**

Yohana 3:16

**kitani nzuri ya kusokota – Yesu.**

---

## Vifuniko vya hekalu:

**Samawi (bluu) huwakilisha Utii wake**

**Nena na wana wa Israeli, na kuwaagiza ya kwamba wajifanyie vishada katika ncha za nguo zao, katika vizazi vyao, tena ya kwamba watie katika kila kishada cha kila ncha nyuzi za rangi ya samawi;**

Hesabu 15:38,39

**tena, alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba.**

Filipi 2:8

---

## Vifuniko vya hekalu:

**Kwa kuwa katika yeye vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi, vinavyoonekana na visivyoonekana; ikiwa ni vitu vya enzi, au usultani, au enzi, au mamlaka; vitu vyote viliumbwa kwa njia yake, na kwa ajili yake.**

Kolosai 1:16

**Zambarau huwakilisha ukuu wake**

## Vifuniko vya hekalu:

*Nyuesi – Huwakilisha dhambi (1 Yohana 1:5)*

*Na hii ndiyo habari tuliyoisikia kwake, na kuihubiri kwenu, ya kwamba Mungu ni nuru, wala giza lo lote hamna ndani yake.*

## Vifuniko vya hekalu:

- **Singa za mbuzi.**

**na nyuzi za rangi ya samawi, na za rangi ya zambarau, na za rangi *nyekundu*, na nguo za kitani safi, na *singa za mbuzi;***

**Kutoka 25:4**

HUWAKILISHA- USAFI

## Vifuniko vya hekalu:

- **Ngozi za kondoo.**

**na ngozi za kondoo waume zilizotiwa rangi nyekundu, na ngozi za pomboo, na miti ya mshita,**

**Kutoka 25:5**

HUWAKILISHA DAMU YA YESU

Siku ya pili yake amwona Yesu anakuja kwake, akasema, Tazama, Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu!

Yohana 1:29

## Vifuniko vya hekalu:

- **Ngozi za pomboo.**

**na ngozi za kondoo waume zilizotiwa rangi nyekundu, na ngozi za pomboo, na miti ya mshita,**

**Kutoka 25:5**

HUONESHA JINSI YESU ALIVYOUFUNIKA UUNGU KWA UBINADAMU

## MADINI YALIYOTUMIKA

1. *Dhahabu – huwakilisha Utukufu wa mbinguni (Ufunuo 3:18)*

*Nakupa shauri, ununue kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto, upate kuwa tajiri, na mavazi meupe upate kuvaa, aibu ya uchi wako isionekane, na dawa ya macho ya kujipaka macho yako, upate kuona.*

## MADINI YALIYOTUMIKA

*Fedha – huwakilsha ukombozi wenye gharama isiyopimika (1 Petro 1:18)*

*Nanyi mfahamu kwamba mlikombolewa si kwa vitu viharibikavyo, kwa fedha au dhahabu; mpate kutoka katika mwenendo wenu usiofaa mlioupokea kwa baba zenu; bali kwa damu ya thamani, kama ya mwana-kondoo asiye na ila, asiye na waa, yaani, ya Kristo.*


## MADINI YALIYOTUMIKA

*Shaba – Huwakilisha Uungu duniani (Filipi 2:5-8)*

*Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu; ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho; bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu; tena, alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba.*

## *Mafungu ya kukariri:*

- *1 Yohana 1:9 - Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.*
- *Danieli 8:14 - Akamwambia, Hata nyakati za jioni na asubuhi elfu mbili na mia tatu; ndipo patakatifu patakapotakaswa.*
- *Kutoka 25:8 - Nao na wanifanyie patakatifu; ili nipate kukaa kati yao.*
- *Ebrania 4:14-16 - Basi, iwapo tunaye kuhani mkuu aliyeingia katika mbingu, Yesu, Mwana wa Mungu, na tuyashike sana maungamo yetu. Kwa kuwa hamna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu; bali yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi. Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji.*




## MAANA YA VITU VILIVYOKUWA NDANI YA HEKALU

## Geti (lango kuu)

Zaburi 15:1-2


Bwana, ni nani atakayekaa Katika hema yako? Ni nani atakayefanya maskani yake Katika kilima chako kitakatifu? Ni mtu aendaye kwa ukamilifu, Na kutenda haki. Asemaye kweli kwa moyo wake,





## Madhabahu ya kafara

- *Ilitengenezwa kwa mti wa mshita.*
- *Ilifunukwa kwa shaba.*
- *Ilikuwa ya mraba.*
- *Kona zake nne zilikuwa na pembe kama za mnyama.*
- *Hapa ndipo zilipotolewa kafara zote.*



## Madhabahu ya kafara

Yohana 1:29

***Siku ya pili yake amwona Yesu anakuja kwake, akasema, Tazama, Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu!***




Birika la maji
Kutoka 29:4
Kisha mlete Haruni na wanawe hata mlangoni pa hema ya kukutania, ukawaoshe kwa maji.
Laver


Birika la maji
Na Haruni na wanawe wataosha mikono yao na miguu yao humo; hapo waingiapo ndani ya hema ya kukutania; watajiosha majini, ili wasife; au hapo watakapoikaribia madhabahu ili watumike, kumteketezea Bwana sadaka ya moto; basi wataosha mikono yao na miguu yao ili kwamba wasife; na neno hili litakuwa amri kwao milele, kwake yeye na kwa wazao wake katika vizazi vyao vyote.
Kutoka 30:19-21
Laver


Birika la maji
Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake; ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno;
Efeso 5:25-26
Laver


Yesu ndiye atuoshaye dhambi zetu.


Hema ya kukutania
wala tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine; bali tuonyane; na kuzidi kufanya hivyo, kwa kadiri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia. Waebrania 10:25


PATAKATIFU
NA
PATAKATIFU PA
PATAKATIFU

## Kinara cha taa

- *Kilitengenezwa dhahabu tupu. (kutoka 25:31)*
- *Kilikuwa na vinara saba vya taa.*
- *Juu yake paliwekwa mafuta ya zeituni ili kukiwasha.*
- *Kiliwaka muda wote.*

Zaburi 119:105
Yohana 8:12
Yohana 12:46




## Kinara cha taa

**Neno lako ni taa ya miguu yangu, Na mwanga wa njia yangu.**

Zaburi 119:105


**Mimi nimekuja ili niwe nuru ya ulimwengu, ili kila mtu aniaminiye mimi asikae gizani.**

Yohana 12:46



## Kinara cha taa

**Basi Yesu akawaambia tena akasema, Mimi ndimi nuru ya ulimwengu, yeye anifuataye hatakwenda gizani kamwe, bali atakuwa na nuru ya uzima.** Yohana 8:12



## Kinara cha taa

**Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji hauwezi kusitirika ukiwa juu ya mlima. Wala watu hawawashi taa na kuiweka chini ya pishi, bali juu ya kiango; nayo yawaangaza wote waliomo nyumbani. Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni.**

Mathayo 5:14-16

**mpate kuwa wana wa Mungu wasio na lawama, wala udanganyifu, wasio na ila kati ya kizazi chenye ukaidi, kilichopotoka; ambao kati ya hao mnaonekana kuwa kama mianga katika ulimwengu,**

Wafilipi 2:15



## Meza ya mikate ya wonyesho


- *Ilitengenezwa kwa mti wa mshita. (kutoka 25:23)*
- *Ilifunukwa kwa dhahabu.*
- *Juu yake palikwa na mikate 12.*
- *Pia palikuwa na vikombe vya divai.*



## Meza ya mikate ya wonyesho

**Naye akajibu akasema, Imeandikwa, Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu.**


Mathayo 4:4



## Meza ya mikate ya wonyesho

Mimi ndimi chakula chenye uzima kilichoshuka kutoka mbinguni; mtu akila chakula hiki, ataishi milele. Na chakula nitakachotoa mimi ni mwili wangu, kwa ajili ya uzima wa ulimwengu.


Yohana 6:51



## Meza ya mikate ya wonyesho


*Kwa maana chakula cha Mungu ni kile kishukacho kutoka mbinguni na kuupa ulimwengu uzima.*

Yohana 6:33




## Madhabahu ya kufukiza uvumba


- *Ilitengenezwa kwa mti wa mshita. (kutoka 30:1-3)*
- *Ilifunukwa kwa dhahabu.*
- *Juu yake palifukizwa uvumba.*
- *Ilifanyika mara moja kwa siku.*



## Madhabahu ya kufukiza uvumba

Na malaika mwingine akaja akasimama mbele ya madhabahu, mwenye chetezo cha dhahabu, akapewa uvumba mwingi, ili autie pamoja na maombi ya watakatifu wote juu ya madhabahu ya dhahabu, iliyo mbele ya kiti cha enzi.

Ufunuo 8:3



## Madhabahu ya kufukiza uvumba

…kila mmoja wao ana kinubi, na vitasa vya dhahabu vilivyojaa manukato, ambayo ni maombi ya watakatifu.

Ufunuo 5:8



## Meza ya mikate ya wonyesho

*Kadhalika Roho naye hutusaidia udhaifu wetu, kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo, lakini Roho mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa.*


Warumi 8:26



## Sanduku la agano

- *Kilitengenezwa mti wa mshita. (kutoka 25:10-11)*
- *Juu yake palikuwa na kiti cha rehema, pamoja na makerubi yaliyokifunika.*
- *Ndani yake palikuwa na mbao mbili za mawe zenye amri kumi za Mungu, fimbo ya haruni iliyochipua, na kopo lenye manna*
- *Pembeni yake palikuwa na sheria za Musa.*







## Meza ya mikate ya wonyesho

***Kwa kuwa torati ilitolewa kwa mkono wa Musa; neema na kweli zilikuja kwa mkono wa Yesu Kristo.***

Yohana 1:17




## Kabila ya lawi

- Kabila ya Lawi ndiko walikotoka makuhani
- Makuhani hawa walikuwa na mavazi yao ya pekee

## Soma kitabu cha Pambano kuu kuhusu hukumu ya upelelezi






## Wanyama alioletwa kwa ajili ya kafara za kila siku

Sadaka za kuteketezwa (ng'ombe dume, mbuzi asiye na mawaa, kondoo,au ndege)

Walawi 1:1-17




Sadaka zilizoletwa kwa ajili ya kafara za kila siku
Nafaka.
Walawi 2:1-16


Wanyama alioletwa kwa ajili ya kafara za kila siku
Sadaka za Amani (kondoo au mbuzi)
Walawi 3:1-17


Wanyama alioletwa kwa ajili ya kafara za kila siku
Sadaka ya dhambi (ng'ombe mume, mbuzi au kondoo)
Walawi 4:1-35